

# Usawiri wa moyo kama mhimili wa epistemolojia ya Wabantu kuhusu ontolojia ya mtu: Mjadala kutoka riwaya za Euphrase Kezilahabi

## Athumani Ponera

Chuo Kikuu cha Dodoma (University of Dodoma, Tanzania)

E-mail: [athuman.ponera@udom.ac.tz](mailto:athuman.ponera@udom.ac.tz)

## Issaya Lupogo

Chuo Kikuu Mzumbe (Mzumbe University, Tanzania)

E-mail: [islupogo@mzumbe.ac.tz](mailto:islupogo@mzumbe.ac.tz)

## IKISIRI

Makala hii inachagizwa na swali: Moyo una thamani gani kwa Wabantu katika kutambua na kubainisha kuwapo kwa mtu? Katika kujibu swali hili, makala inajiegemeza katika matawi mawili ya falsafa—ontolojia na epistemolojia. Hoja kuu ya makala ni kuthibitisha namna moyo unavyosimama kama mhimili mmojawapo wa epistemolojia ya Wabantu kuhusu ontolojia ya mtu. Utafiti uliozaa makala hii ulifanywa kwa kutumia Nadharia ya Epistemolojia. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa maandiko. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba Wabantu wanauthamini moyo kama kibainishi cha mtu kiontolojia; pia ni kielelezo cha kiepistemolojia ambapo kazi yake kubwa ni kumwongoza mtu kufanya

tafakuri kuhusu ulimwengu wake. Hii inamaanisha kwamba, kwa Wabantu, fikra hujengwa moyoni na si akilini. Hatimaye, makala hii imethibitisha kwamba moyo alionao mtu ndio hubeba tabia yake kwa jumla. Kupitia kudhihirisha tabia hiyo, moyo hubeba dhima muhimu ya kusimama kama mhimili wa kumtofautisha mtu-kweli na si-mtu. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa, kupitia utendaji unaosababishwa na moyo, mtu huweza kuiimarisha au kuidhoofisha kani-uhai; hivyo kuwa zana ya kiontolojia. Ithibati za hoja hizi zimetolewa katika riwaya teule za Euphrase Kezilahabi, mwandishi kutoka Tanzania.

**Dhana muhimu:** epistemolojia, ontolojia, Wabantu, mtu, binadamu, moyo

## CITATION

Ponera, A. & Lupogo, I. (2024). Usawiri wa moyo kama mhimili wa epistemolojia ya Wabantu kuhusu ontolojia ya mtu: Mjadala kutoka riwaya za Euphrase Kezilahabi. *Journal for Language Teaching*, 58(1), Article 6549. <https://doi.org/10.56285/jltVol58iss1a6549>

# Depiction of the heart as a pillar of Bantu epistemology on the ontological features of a person: A case of Euphrase Kezilahabi's novels

## ABSTRACT

This paper hinges on the question: What is the value of a heart for Bantu people in recognising and realising a person's being? Based on this question, this paper relies on two branches of philosophy—ontology and epistemology. The central argument of this paper is to justify how the heart stands as one of the pillars of Bantu epistemology about the ontological features of a person. The research was guided by epistemology theory. Data were collected through document analysis. The results show that Bantu people regard and respect the heart as the ontological determining element of the person; also, it is viewed as an epistemological identity in which its main role is to guide a person to think critically about his/her world. This means that Bantu people use the heart (instead of the brain) to think. Finally, this paper has confirmed that the heart carries the behaviour of the Bantu people. Therefore, based on that reality, the heart is the critical factor that differentiates a good from a bad person. Based on that heart's function, a person can strengthen or weaken his/her 'vital force'. These arguments are justified by the selected Euphrase Kezilahabi's novels.

**Keywords:** epistemology; ontology; Bantu people; person; human; heart

## 1. Utangulizi

Ayers (1991) anaeleza kuwa ontolojia huchunguza kuhusu kuwako kwa ulimwengu na vilivyomo. Griswold (2001) anaongeza kuwa ontolojia ni tawi la falsafa linaloshughulikia kuwapo na kuishi kwa mtu. Ontolojia ina vitapo muhimu viwili, kosmolojia na eskatolojia. Kwa mujibu wa Mtega (2023), kosmolojia hujihusisha na chanzo cha kuwapo kwa mtu hadi mauko yake (kuzaliwa, kuishi, na kufa) na eskatolojia hujihusisha na mambo yanayomhusu mtu baada ya kifo (Duwe, 2022). Ontolojia ya Wabantu ni seti ya maelezo kuhusu asili ya kuwapo kwa Wabantu na mtazamo wao kuhusu kuwapo kwao, maisha yao, utangamano wao, na ulimwengu kwa ujumla (Mbiti, 1995). Wanaontolojia hujishughulisha kujibu maswali yafuatayo: mtu ni nani? Asili ya mtu ni nini? Asili ya ulimwengu ni nini? Kuwako ni nini? Kuwako huanzaje? Vilivyoko ni vipi na vilivyokuwapo au vinavyosemekana kuwapo ni vipi? Vilivyoko

vinahusianaje na vilivyokuwapo? Vilivyoko vinafanana au kutofautianaje na vilivyokuwapo? (Mbiti, 1995; Mihanjo, 2004).

Majibu ya maswali haya ni sehemu ya taarifa, maarifa, na uzoefu unaokuwa katika akili za wanajamii. Taarifa au maarifa hayo hupatikana kwa kufikiri. Hali hii inaibua hoja kuwa suala hili la kuwapo huhitaji fikra au tafakuri; hapo ndipo unapochimbuka muumano wa ontolojia na epistemolojia.

Kwa mujibu wa Kaphagawani na Malherbe (2003), epistemolojia ni tawi la falsafa ambalo msingi wake mkuu ni kuchambua na kutathmini madai kuhusu maarifa. Kwa kuwa watu wote wana uwezo wa kujua, epistemolojia ni ya kijumla licha ya tofauti katika utamaduni, makabila, rangi au utaifa. Hata hivyo, namna za kuyafikia maarifa na misingi ya madai ya kuwa nayo hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Namna ambavyo Mwafrika anajua, au anatoa madai ya kujua ni tofauti na Mchina au Mzungu. Kwa maana hiyo, namna Waafrika wanavyofikiri au kuutazama ulimwengu wao ni tofauti na wale wasio Waafrika (Mbiti, 1995; Onyeowuenyi, 1995). Kwa maneno mengine, ingawa epistemolojia kama taaluma inayohusu maarifa ni ya kijumla, njia za kupata maarifa zinatofautiana kutokana na tofauti za miktadha ya jamii moja na nyingine. Epistemolojia ya Wabantu hujumuisha mambo yanayochukuliwa kuwa ya jumla kuhusu maarifa na ujuzi wa Wabantu. Dhana hii tunaitumia katika makala hii, huku tukiwa na uhakika kuwa kuna tofauti kubwa miongoni mwa tamaduni nyingi barani Afrika. Uchunguzi wa epistemolojia hujishughulisha na ukweli, uhalisi, imani, mawazo, welewa, pamoja na uzoefu au tajiriba za watu. Kizio cha msingi cha kushugulikia mambo hayo ni kufikiri kimantiki.

Kuna uhusiano wa karibu sana baina ya matawi haya mawili (ontolojia na epistemolojia), chambilecho Khamis (2022) kuwa ni vigumu kuichambua epistemolojia bila kuhusisha ontolojia. Fikra hii inayakinishwa na hoja kuwa matawi yote haya yanamhusu mtu. Ni vigumu kwa uchambuzi wa kifalsafa kuanza na akijuacho mtu, bali huanza na kuwako kwa mtu mwenyewe. Zaidi, Chuachua (2016) anatuyakinishia kuwa ushikamani wa matawi haya unatokana na ukweli kuwa uzito na thamani ya kiepistemolojia huhusiana sana na darajia au mkufu wa kiontolojia. Mathalani, akijuacho mzee huwa na uzito na thamani kuliko akijuacho mtoto. Hii ni kwa sababu mzee yuko katika kidato cha juu cha kiontolojia au yuko kwenye nukta ya juu ya mkufu wa kiontolojia kuliko mtoto.

Epistemolojia na ontolojia, kama yalivyo matawi mengine ya falsafa, huwa na hali ya ujumla, yaani kutandawaa katika eneo pana, hususani kwa jamii zinazoendana (siyo kulandana) kwa mambo mengi kama ilivyo kwa Wabantu (Chuachua, 2016). Makala hii inatalii ontolojia na epistemolojia ya Wabantu. Kwa mujibu wa Chuachua (2011, 2016), dhana ya Wabantu humaanisha jamii mbalimbali za watu wanaopatikana Kusini mwa Jangwa la Sahara. Sehemu kubwa ya watu wa jamii hizi ina rangi nyeusi. Pia, sehemu kubwa ya watu wa jamii za Wabantu ina utamaduni unaoendana; hivyo pia kuendana katika vipengele vya falsafa (kama vile ontolojia na epistemolojia).

Maarifa ya Wabantu hutegemea mfuatano wa kiontolojia unaounda duara la maisha. Mfuatano huu unaojiegemeza katika wigo wa kani-uhai, ndio msingi mkuu wa mawanda ya kiepistemolojia. Sababu za kusema hivi ni kuwa, ‘kujua’ kwa upande wa Wabantu kunadhihirika kiontolojia. Mwenye mawazo kuhusu historia ya vizazi na namna ya kuimarisha kani-uhai ndiye anayejua zaidi, na kwa mantiki hiyo, ndiye mwenye maarifa.

Ipo mifano ya kutosha kutoka katika jamii za Wabantu kuwa ukweli au uhalisi wa maarifa kuhusu jambo fulani huongezeka kila lisemwapo na mtu aliye na umri mkubwa, yaani mzee zaidi. Onyeowuenyi (1995) anaeleza kuwa suala la maarifa lina uhusiano mkubwa na ontolojia; na kwamba, mtazamo wa Wabantu kuhusu maarifa yao hautofautiani na ule wa kimetafizikia. Maarifa au busara kwa Wabantu huhusiana na kiwango cha welewa kuhusu asili ya kani-uhai na mwingiliano wake. Tempels (1959:73) anatueleza kuwa, “hekima au busara za kweli zinategemea maarifa ya kiontolojia; ni maarifa kuhusu kani-uhai za mfuatano wa vizazi, muungano na mwingiliano wake”. Onyeowuenyi (ameshatajwa) anaongeza kuwa: “mtu anaonekana kuwa anajua au ana hekima ama busara kila anavyozeeka (uk. 41).” Kwa mtazamo huo, wahenga wana busara au maarifa zaidi, wakifuatiwa na wazee walio hai. Chanzo cha maarifa kwa Wabantu si kuwa na elimu kubwa ya shuleni kama wafikiriavyo wasio Wabantu. Elimu ipatikanayo shule haina uhusiano na busara au maarifa ambayo Wabantu huyathamini. Wabantu wanaamini kuwa wakati wote wazee na wahenga ndio wenye maarifa, kwa kuwa ndio wenye sifa na uwezo wa kuwaunganisha watu na Mungu wao.

Tumedokeza hapo awali kuwa matawi mawili yanayojadiliwa katika makala hii yanamhusu mtu. Maswali muhimu ni kuwa, ‘mtu ni nini?’ na ‘kuna tofauti gani kati ya mtu na binadamu?’ Dhana hizi mbili—mtu na binadamu—ni tofauti. Kwa muktadha wa kifalsafa, binadamu ni kiumbe wa kibayolojia mwenye utashi, ilhali mtu “ni kiumbe

ajibainishaye kwa uchangamani na mwenendo wake katika jamii” (Adeofe, 2001:72). Hii inamaanisha kuwa watu wote ni binadamu, bali si binadamu wote ambao wanaweza kuwa watu.

Dhana ya mtu na utu wake imejadiliwa kwa kina na watafiti mbalimbali, wakiwamo Tempels (1959), Wiredu (1980), Gbadegesin (1984; 1991), Kagame (1989), Mbiti (1995), Gyekye (1995), Appiah (1992), Adeofe (2001), na Kaphagawani (2004). Wataalamu hawa wanaonesha vigezo mbalimbali vinavyoweza kumbainisha mtu. Hata hivyo, wote wana mawazo sawa kuhusu vigezo viwili ambavyo ni mwili na roho. Kwa mujibu wa Kaphagawani (ameshatajwa), Waakan wa nchini Ghana huuita mwili *nipadua*, wakati roho huiita *okra*. Gbadegesin (1991) na Hallen na Sodipo (1997) wanaongeza kuwa Wayoruba wa Nigeria huuita mwili *ara* na roho huiita *emi*. Vigezo vingine ambavyo jamii za Wabantu huvitumia kumpambanua mtu ni haiba, kichwa, moyo, kani toka kwa Mungu, pamoja na damu (Gyekye, ameshatajwa na Appiah, ameshatajwa). Maoni ya wataalamu hawa yanadokeza umuhimu wa kuchunguza mawazo ya kifalsafa ya Wabantu kwa kuhusisha dhana hii ya roho. Inaonekana wazi kuwa roho ni kipengele muhimu cha kiontolojia; na ndicho kitambulishi cha mtu. Wakati maoni ya wataalamu waliotajwa yanataja dhana ya ‘roho’ tunaweka msisitizo kuwa kuna mwingiliano mkubwa miongoni mwa Wabantu katika kutaja na kutumia maneno mawili, ‘roho’ na ‘moyo’. Mkanganyo huu unaweza kudhihirika kupitia matumizi ya lugha ya kawaida (katika mazungumzo). Mathalani, Waswahili wana msemu, “...ana moyo mzuri/ana roho nzuri”. Katika maongezi ya kawaida, kutamkwa kwa neno lolote kati ya hayo humaanisha mwelekeo uleule wa kitabia.

Mjadala na maoni ya wataalamu hao yanatufikisha katika kujiuliza, “Wabantu humwangaliaje mtu?” Kuhusu swali hili, Adeofe (2001:69) anatutaka tuanze kujiuliza: Mtu ni nani? Kitu gani kinamfanya mtu awe alivyo? Ni mambo yepi ya kiontolojia humjenga mtu? Adeofe (ameshatajwa) anaongeza kuwa Wabantu wanaonekana kufikiri kuwa kuna sehemu za kimetafizikia katika viungo mbalimbali vya mwili, hususani, kichwa, moyo, na utumbo.

Kila jamii ina mitazamo inayomwelezea mtu, yaani mawazo yanayoelezea mambo yanayomfanya mtu awe kama alivyo. Mitazamo hiyo inaweza kuhusisha mambo kadhaa. Kwa mfano, Appiah (1992) anaeleza kuwa mawazo ya watu wa jamii nyingi za barani Amerika humtazama na kumwelezea mtu kwa vigezo vya: woga, tumaini, imani, dhamira, hamu, wivu, na huruma. Haya yote huwekwa pamoja kwa namna inayoonesha uhusiano kati ya matukio ya ndani ya watu wenyewe ambayo huwafanya

watende, sababu ya kutenda, pamoja na miili yao inayotenda. Kitovu cha mifanyiko ya dhamiri na matendo yanayodhihirisha dhamiri hizo ni fikra. Kwa hiyo, mwelekeo wa jumla wa jamii hizo kuhusu ‘gia’ inayomjenga mtu katika jamii yao ni ubongo; yaani fikra huzalishwa ubongoni.

Ni wazi kuwa mfano huu wa Kimagharibi wa mtazamo kuhusu mtu unakinzana na ule wa jamii za Wabantu. Akitudokezea kuhusu tofauti hizo, Appiah (ameshatajwa) anaeleza: “*In other societies, it has been not the brain but the breast that has been thought of as the home of many of the most important states that make people act* (uk. 25).” Anamaanisha kuwa, “Katika jamii nyingine, inaonekana kuwa kifua ndiyo sehemu ambayo michakato mingi ya mwili wa binadamu inayowafanya watu watende hutokea na siyo katika ubongo... (tafsiri yetu).

Wakati vitovu vya fikra za watu wa jamii nyingine vikiwa ubongo au vifua, kwa Wabantu kitovu chao ni kipi? Kujua kwao kwa ujumla kunaukiliwa na nini? Wanaujaje ulimwengu wao? Kujua kuhusu kuwapo kwao kunaukiliwa na nini? Sehemu ya tatu ya makala hii inatoa majibu ya maswali haya yaliyodokezwa.

## 2. Nadharia na Methodolojia Iliyotumika

Utafiti uliozalisha makala hii uliongozwa na Nadharia ya Epistemolojia. Kwa mujibu wa Kasprisin (1987) na Chuachua (2016), mbali na epistemolojia kuwa tawi la falsafa, ni umbo kamili linalotumika kama mkabala na nadharia ya kushughulikia kazi za fasihi. Hii ni kwa sababu ina dhana, misingi, na dira mahususi ambayo watafiti au wahakiki huweza kuitumia katika kushughulikia masuala mbalimbali ya kiuchambuzi/kiutafiti.

Anthony (2009) na Newman (2023) wanaeleza kuwa René Descartes ndiye mwasisi wa Nadharia ya Epistemolojia. Mwanafalsafa huyu anatajwa kama mwanazuoni aliyefanya mageuzi makubwa katika uga wa epistemolojia, ikiwamo kupanua mawanda kutoka kuutazama kama dhana tu hadi kuiona kama nadharia ya maarifa inayoweza kusimama kama nyenzo ya kuchambulia masuala mengine yanayohusiana na maisha ya mwanadamu (Cottingham, 2010). Descartes (1641) anaelezwa katika Cottingham (2017) kuwa alijipatia umaarufu kupitia kaulimbiu yake ya ‘*Cogito, ergo sum*’. Ponera na Mkomwa (2019) wanafafanua kuwa kaulimbinu hii inayotokana na lugha ya Kifaransa (*Je pense, donc, je suis*) ikimaanisha “Ninafikiri, ndiyo maana nipo hivi” imejenga msingi imara wa mwanadamu kufikiri kitunduizi kuhusu masuala mbalimbali yanayomzunguka. Hivyo, kaulimbinu hii inatungazia muumano baina ya kuwapo kwa

mtu na kufikiri; na kwamba, *cogito*—ninafikiri (kufikiri)—ndio msingi wa maarifa. Kwa ujumla, dhana zinazojenga mawanda ya nadharia hii ni: kujua, kuamini, kufikiri, jinsi ya kujua, pamoja na mipaka ya kujua (Cottingham, 2010; Newman, 2023).

Kwa mujibu wa Stumpf na Abel (2002), Cottingham (2010) na Chuachua (2016), ifuatayo ni misingi ya nadharia hii:

- a) Maarifa hupatikana kutokana na kujua na tajiriba;
- b) Kujua ni mchakato unaohusisha milango ya fahamu;
- c) Vyanzo vya kujua hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Mathalani, jamii nyingi za Afrika hujua kwa kutumia maono na maoni ya wazee na wahenga;
- d) Maarifa ni mali ya jamii; na
- e) Maarifa ya binadamu yana mipaka. Stumpf na Abel (2002:26) wanasisitiza kuwa, “hata kama tunaweza kupata maarifa, bado mawanda ya maarifa yetu yana mipaka ya kijiografia na kinyakati”. Wanamaanisha kuwa, hakuna mtu anayeweza kusema kuwa anajua kila kitu hapa duniani. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mtu huyo anakabiliwa na mipaka ya kiitikeli, kiuchumi, kisiasa, kijografia, kijamii, na kiutamaduni.

Nadharia hii ilituongoza kukusanya data na kujadili matokeo ya utafiti kwa kuzingatia misingi hii. Msingi (a) ulituongoza kujiuliza kuhusu maana ya maarifa. Hivyo, ulisaidia kujibu mojawapo ya maswali yetu madogo lililouliza, ‘Wabantu wanaujuaje ulimwengu wao?’ Msingi (b) ulituongoza kuzingatia kuwa kujua ni mchakato unaohusisha milango ya fahamu. Hivyo, tumeichukulia dhana ya kujua katika makala hii kama tokeo la juhudi fulani. Hii inamaanisha kuwa msingi huu umesaidia kujibu swali dogo la ‘kujua kwa Wabantu kwa ujumla kunaukiliwa na nini?’ Msingi (c) ulituongoza kuzingatia kuwa kila jamii ina namna yake ya kupata maarifa. Hivyo, ulisadia kupatikana kwa majibu ya maswali kama vile, ‘kitovu cha fikra za Wabantu ni kipi?’, na ‘kujua kwa Wabantu kwa ujumla kunaukiliwa na nini?’ Msingi (d) ulituongoza kuzingatia kuwa maarifa na ujuzi ni jambo la wanajamii wote. Hivyo, majibu ya swali la ‘Wabantu wanaujuaje ulimwengu wao?’ yalishamirishwa na fikra za msingi huu. Msingi (e) ulituongoza kuzingatia kuwa mtu hujua mambo machache, na kwamba, watu hutofautiana katika mambo wayajuayo. Aidha, msingi huu ulisaidia kujibu swali lililodokezwa katika msingi (d). Kwa ujumla, kujibiwa kwa maswali hayo madogomadogo kupitia misingi hiyo iliyoelezwa, hatimaye, kulifanikisha kujibiwa kwa swali kuu lililoshikilia kiini cha

makala hii kuwa, ‘Moyo una thamani gani kwa Wabantu katika kutambua na kubainisha kuwapo kwa mtu?’

Kwa upande wa methodolojia iliyotumika, data za utafiti uliozaa makala hii zilipatikana kwa njia ya uchambuzi wa maandiko. Watafiti walisoma na kuchambua maandiko mbalimbali yanayohusiana na ontolojia, epistemolojia, na dhana ya mtu kwa ujumla. Vilevile, walisoma na kuchambua riwaya teule ambazo ni *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007), *Nagona* (2011), pamoja na *Mzingile* (2011). Riwaya hizi tatu ziliteuliwa kama sampuli ya kazi mbalimbali za Euphrase Kezilahabi zinazowasilisha maudhui mbalimbali kuhusu mtu. Riwaya hizi zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa, ambapo kupitia usomaji wa awali waandishi waliona ujichomozaji wa fikra zenye upekee kuhusu dhana za moyo na mtu.

Mbinu iliyotumika kuchanganua data zilizopatikana ni usimbishaji wa maudhui. Hii ni miongoni mwa mbinu muafaka za kuchanganulia data za kitaamuli. Kupitia mbinu hii, data zilizopatikana zilipangwa katika makundi mbalimbali ambayo yalipewa hadhi ya misimbo. Kila msimbo uliwakilisha maana yenye mwelekeo wa kujibu mojawapo au baadhi ya maswali madogomadogo yaliyokwishadokezwa katika kurasa zilizotangulia. Kisha, misimbo hiyo ilihusishwa ili kuibua ruwaza mpya ya maana kuhusiana na swali kuu la ‘Moyo una thamani gani kwa Wabantu katika kutambua na kubainisha kuwapo kwa mtu?’

### 3. Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inawasilisha matokeo kuhusu namna Wabantu wanavyouthamini moyo kama nyenzo muhimu ya kufikiri kuhusu kuwapo kwao. Sehemu hii inaundwa na vijisehemu viwili—maelezo mafupi kuhusu riwaya teule pamoja na thamani ya moyo kama mhimili wa epistemolojia ya Wabantu kuhusu ontolojia yao.

#### 3.1 Maelezo Mafupi kuhusu Riwaya Teule

Riwaya zinazoelezwa hapa ni *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007), *Nagona* (2011), pamoja na *Mzingile* (2011). Zote hizi ni riwaya zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Huyu ni mwandishi aliyezaliwa tarehe 13/4/1944 kijijini Namagondo, Ukerewe, Tanzania. Mbali na uandishi, Kezilahabi alikuwa profesa wa taaluma mbalimbali za fasihi. Alifariki tarehe 9/1/2020 na kuzikwa katika kijiji hichohicho alichozaliwa.



Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1975. Katika jalada lake la nyuma, mwandishi anatupatia muhtasari wa maudhui yake kama ifuatavyo:

*Dunia Uwanja wa Fujo* ni riwaya inayosimulia kisa cha Tumaini, kijana anayekulia katika mazingira ya utajiri na katika kijiji kilichoghoshi umasikini, ushirikina na vituko, kabla ya kuhamia mjini na kukumbana na ulimwengu tofauti na aliouzoa. Ni riwaya inayoonesha jinsi maisha ya Tumaini yanavyoingiliana na wahusika wengine katika jamii yake inayokumbwa na mabadiliko ya kijamii na kisiasa. Hii ni riwaya inayoonesha jinsi msako wa furaha maishani unavyoweza kukumbwa na kila aina ya vikwazo na namna swala la malezi lilivyo changamoto katika jamii ya leo.

Maelezo hayo yana msaada mkubwa sana katika kutuonesha maudhui ya jumla ya kitabu hiki. Riwaya hii inayamulika maisha halisi ya Mbantuu tangu kuzaliwa kwake hadi kufa. Kwa mujibu wa Mbatiah (1998), kwa kiwango fulani, riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* inaendeleza mijadala kuhusu uduni wa mwanadamu pamoja na tatizo la maisha inayoanzia katika riwaya nyingine ya Kezilahabi iitwayo *Kichwamaji* (2008).

Ufafanuzi anaotoa mtunzi kuhusu dhana ya ‘dunia uwanja wa fujo’ unatusaidia kuelewa riwaya hii katika mawanda mapana ya kiutunzi. Anasema:

Zamani, niliamini kwamba kila mwanadamu ameumbwa kuja hapa duniani ili apate kufurahia ulimwengu kiasi awezavyo kabla hajafa. Lakini sasa ninaamini kwamba Dunia Uwanja wa Fujo. Kila mwanadamu ameumbwa kuja kufanya fujo yake halafu anajiondokea na kupotea. Kuna fujo za aina nyingi. Watu wengine wamefanya fujo zaidi ya wengine (uk. 63).

Ufafanuzi huu una viashiria vya kiontolojia, hususani suala la kuwapo kwa mwanadamu duniani (malengo ya kuwapo kwake na matendo mbalimbali anayofanya). Riwaya hii inayaona maisha ya binadamu yanafanana na ya mtu aliye katika safari ya kuitafuta kweli katika maisha yake. Katika kuisawiri hali hiyo, mwandishi anaonesha kuwa mwanadamu huranda huku na huko kifikra juu ya maisha yake. Anasema:

Zamani nilifikiri kwamba mwanadamu ndiye kiumbe peke yake mwenye furaha na uhuru. Sasa nimeona kwamba kati ya viumbe, mwanadamu ni wa mwisho katika mambo haya mawili... Mara nyingi huwa nakwenda shamba na gari langu. Peke yangu huwa nakaa chini ya mti na kufikiri... najjuliza nini kweli maana ya maisha (uk. 64).

Kuishi kunakodokezwa hapa ni fikra ya kiontolojia. Miongoni mwa mihimili ambayo Kezilahabi ameitumia kufafanua fikra hizo za kiontolojia ni moyo, kama inavyojadiliwa katika kijisehemu kifuatacho cha makala hii.

Riwaya ya pili ni *Nagona*. Hii ni riwaya iliyochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1990. Baada ya kuchapishwa kwa kazi hii, mwaka 1991 riwaya nyingine ya *Mzingile* ilichapishwa. Kiini cha maudhui katika riwaya zote hizi mbili hakitofautiani. Zote zinajadili dhana ya kutafuta ukweli katika maisha. Katika riwaya zote mbili, ukweli huo umepewa taswira ya mwanga.

Riwaya hizi mbili zinajadili hadhi na utu wa Mwafrika dhidi ya kasumba za kigeni. Mwandishi anaonesha kuwa elimu na tamaduni za kigeni ni nyenzo muhimu zinazotumiwa na wageni kumong'onyoa hadhi, utu, tamaduni, na hata historia ya Mwafrika. Kwa kuwa hivi ni viambata vya kuwapo kwa mtu, ni wazi kuwa hapa mwandishi anajadili mustakabali wa ontolojia ya Mwafrika. Kwa kutumia riwaya ya *Nagona*, mwandishi anasisitiza tujenge uwezo wa kufikiri kwa kina ili tuifikie kweli ya maisha (ikiwamo kweli kuhusu kuwapo kwetu). Anaona kuwa, kwa kutofikiri Kiafrika, tunashindwa kujitambua.

Jambo lingine ambalo mwandishi analifikisha kwa hadhira yake kupitia riwaya ya *Nagona* ni chanzo cha maarifa juu ya mambo mbalimbali yanayohusiana na maisha yetu. Anaona kuwa wazee ni chanzo mujarabu kinachoweza kutuongoza kufikiri kuhusu ulimwengu wetu. Anasema:

Babu yangu alijulikana sana kijijini. Wazee wengi walifika mara nyingi jioni kuongea naye. Baadhi walifika kutafuta mawaidha kuhusu migogoro yao, wengine walifika tu kusikiliza hekima yake na masimulizi ya historia ya wakati uliopita. Mara nyingi nilikaa karibu naye kusikiliza maongezi yake na wazee ingawa hapakuwa mahali pangu (uk.15).

Tunamwona Euphrase Kezilahabi katika jitihada za kuielimisha hadhira yake kuhusu umuhimu wa kufikiri na chanzo cha maarifa kuhusu maisha ya sasa na yaliyopita.

Kama ambavyo tayari tumekwisha dokeza katika maelezo ya riwaya ya *Nagona*, riwaya ya *Mzingile* pia imejikita kwenye uwazaji kuhusu ontolojia, ambapo dhana ya uduara katika maisha imetawala tangu mwanzo hadi mwisho. Mpangilio wa matukio na msuko wa uhusika katika riwaya nzima ni wa kiduara. Wahusika wakuu ambao ni Mimi na Mzee wamekuwa wakiachana na kukutana toka mwanzo hadi mwisho. Hali ni hiyo hiyo kwa upande wa wahusika Mimi na mwanamke, pamoja na Kijana na Mimi.

Kwa jumla, riwaya zote tatu—*Dunia Uwanja wa Fujo, Nagona, na Mzingile*—zinajadili suala la ontolojia kupitia dhana ya maisha au kuishi. Maisha yanayojadiliwa katika riwaya hizi yanamhusu mtu. Kwa kuwa riwaya hizi ni za Kiswahili, ni wazi kuwa fikra zinazosawiriwa zinawahusu Waswahili ambao ni sehemu ya Wabantu. Utafiti wetu ulibaini kuwa uwazaji wa Wabantu kuhusu ontolojia ya mtu huegemezwa sana katika moyo. Kijisehemu kifuatacho kinajadili thamani ya moyo kwa Wabantu katika kumtambua na kumbainisha mtu.

### **3.2 Thamani ya Moyo kama Mhimili wa Epistemolojia ya Wabantu kuhusu Ontolojia Yao**

Utafiti wetu ulibaini kuwa Wabantu huuthamini moyo kama kitovu cha kufikiri, kudhamiria, kutenda (kudhihirisha dhamiri), na hatimaye kuamiliana na wanajamii. Tulibaini kuwa moyo, kwa kiasi kikubwa, unaonekana kama kiungo kinachochagiza tafakuri kuhusu ulimwengu; na kwamba, mtu razini ni yule anayezungumza na moyo wake mara kwa mara. Katika aya zifuatazo, tunaonesha data zinazoyakinisha hoja yetu hii kutoka katika riwaya zote tatu zilizotafitiwa.

Katika riwaya ya *Nagona* (Kezilahabi, 2011), mwandishi anaujenga mjadala kuhusu namna moyo unavyosawiri uwazaji wa Wabantu kuhusu ulimwengu wao. Hoja zake zinasisitiza kuwa Wabantu hawaachi kuutaja moyo katika mazungumzo yao ya kawaida. Katika safari ndefu ya kuitafuta kweli ya maisha, ambayo ndani yake mna vikwazo vinavyothibitisha ugumu wa kuutafakari ulimwengu, mwandishi anamtumia mhusika wake mkuu, Mimi, kutueleza kwamba, “mioyo yetu ilikuwa ikidunda kwa subira ya kutaka kujua hicho kikwazo cha mwisho (uk. 59).” Uhusiano wa moyo na akili unaonekana kuwa wa karibu mno na, pengine, kufunika kutambuliwa kwa nafasi ya akili miongoni mwa Wabantu. Tunaelezwa na mwandishi kuwa “moyo ulikuwa unadunda kwa subira ya kutaka kujua.” Hii ina maana kuwa moyo una nafasi kubwa katika utambuzi. Mwandishi anaendelea kutuambia kwamba, “safari hii nilifanikiwa kumshika (paa—ambaye, kwa maoni yetu, katika riwaya hii ametumika kama jazanda ya kweli mbalimbali za maisha). Moyoni nikawa nasema, “Acha nikushike, nikujue siri yako!” (uk. 67, ufafanuzi kwenye mabano ni wetu). Hapa, tunaoneshwa kuwa moyo ni chanzo cha dhamiri ya kutaka kujua na kujua kwenyewe. Kifungu “...safari hii nilifanikiwa kumshika...” kinamaanisha matokeo ya kupata maarifa. Matokeo hayo yamekuja kutokana na jitihada, kama inavyotiliwa nguvu na mhimili wa Nadharia ya Epistemolojia unaosisitiza kuwa kujua ni zao la mchakato unaohusisha milango ya fahamu. Mchakato huo huenda sambamba na ithibati; ndiyo maana katika matini hii

mhusika anathibitisha kwa kumshika. Pamoja na ufafanuzi huo, tunafunuliwa na mwandishi kuwa moyo pia ni chanzo cha ujasiri. Jambo hili tunajuzwa pale Mimi anapoulizwa na mama yake “moyo wako ni mgumu kiasi gani?” (uk. 73).

Katika riwaya ya *Mzingile* (Kezilahabi, 2011), mwandishi anafafanua namna dhana ya moyo inavyodhihirishwa na Wabantu. Kwa kumtumia mhusika wake, Mimi, anatuambia kuwa: “Moyo wa ujasiri, moyo wa udadisi na utundu ulinisukuma mbele ‘...Haidhuru hata kama nikikosea njia; nitauliza huko mbele,’ moyo uliniusia (uk.11). Maelezo haya yanaonesha wazi kuwa tafakuri hufanywa na moyo; na kwamba, Wabantu wanasemezana na mioyo yao. Zaidi, tunafunuliwa kuwa katika safari yake ya kuusaka utu, mwanadamu huwa hajui mambo yote. Hujua baadhi tu, kama tunavyoyakinishiwa na fikra za Nadharia ya Epistemolojia kupitia msingi unaotufahamisha kuwa maarifa ya binadamu yana mipaka.

Pamoja na msisitizo wa mtunzi (Kezilahabi) kuhusu haja ya kutafuta kweli kuhusu maisha, tunaalezwa kuwa jitihada ya kuipata kweli inawezeshwa na moyo. Katika riwaya ya *Mzingile*, anatuieleza:

Nilifikiria namna ya kuifikia nyumba hiyo ambayo haikuonesha kuwa na dirisha. Wakati wote huo sikuona mlango unafunguliwa... Ilikuwa asubuhi nilipoanza jitihada ya kufika kwenye kilele. Moyoni nilikuwa nikijiuliza “Aliyejenga alifikaje?” Maneno haya yalinitia moyo (uk. 17).

Mwongozo huu wa kutafakari maisha unafanywa na moyo wa Mimi, mhusika anayejibainisha kwa hekima na mwongozo mwema wa kifalsafa toka mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Lengo kuu la mwandishi ni kudhihirisha dhana ya kuitafuta kweli kuhusu maisha kwa njia ya kutafakari. Tafakari hiyo inajengwa na moyo badala ya akili.

Mtu mwenye moyo unaomwongoza vema kutafakari ndiye anayejulikana kama mtu-kweli. Hii ndiyo sababu Kezilahabi katika riwaya hii ya *Mzingile* anasema: “ukweli sasa umo katika giza. Nataka uuone kwa mboni za moyo wako (uk. 48).” Hapa, tunaona moyo, kwa namna unavyothaminiwa, umepewa hadi macho (yenye mboni) ili uweze kuona, kumulika, na kuangaza. Kuhusu swali la ‘kwa nini mwandishi ameupa moyo wa Mbantu ogani hiyo ya fahamu—mboni?’, jibu lake linaturudisha kwenye Nadharia ya Epistemolojia kupitia msingi unaodai kuwa kujua ni mchakato unaohusisha kupata uhakika na ithibati kupitia milango ya fahamu (kama vile pua, ngozi, ulimi, masikio, na macho). Hivyo, jazanda hii ya moyo wenye macho inatumulikia umuhimu wa ithibati katika suala zima la kupata au kutumia maarifa na ujuzi.

Jukumu hili la moyo katika kutafakari ulimwengu linaendelezwa na Mimi kwamba, “muda mrefu sasa umepita nikiwa safarini kuwatangazia wanaohusika juu ya kifo chake. Lakini sasa nimechoka. Wazo lenyewe linaanza kuwa jiwe zito juu ya moyo wangu” (uk. 54). Hapa, tunadokezwa pia dhima nyingine ya moyo kama kibebao cha ‘taka za fikra’. Tunaelezwa kuwa mawazo ni mzigo wa moyo; yaani migongano na misongamano ya fikra za mtu kuhusiana na mambo mbalimbali yanayomtokea maishani hubebwa na moyo. Vilevile, kadiri fikra zinapopungua juu ya jambo fulani, hasa kutokana na kuyakaribia mafanikio, ndivyo wepesi wa mzigo moyoni hudhihirika. Mwandishi, kwa kumtumia Mimi, anazidi kutudhihirishia dhima hii ya kiepistemolojia ya moyo. Anatueleza:

Moyo wangu ulikuwa mwepesi sasa. Nilikuwa na furaha ya kuachana na mazingira ya yule mzee, maana sasa nilianza kuhisi kuwa alikuwa akinibanabana sana. Ilikuwa kama kwamba alikuwa ameniwekea duara nilimozunguka bila kutoka nje (uk. 63).

Pamoja na dhana ya wepesi au uzito wa mzigo wa fikra moyoni, msimulizi anatuonesha umuhimu wa kusaka maarifa kutoka kwa wazee wenye hekima, jambo linalotufanya tuwe ndani ya duara. Anasema, “nilikuwa nimesafiri mwendo kiasi. Moyoni nilikuwa nikijiuliza kama kulikuwa na uwezekano wa kutoka nje ya duara ya Mzee (uk. 76).” Tunaendelea kuona dhana hii inavyosawiri uwazaji wa Wabantu. Msisitizo wa umuhimu wa kujifunza maarifa ya Wabantu kupitia maoni na fikra za wazee wenye hekima na busara unatolewa na mwandishi.

Hali hiyo ya Mbantuu kuzungumza na moyo inaoneshwa tena na mtunzi wa riwaya ya *Mzingile* kwa kumtumia Mimi ambaye anasema:

Kijiji changu nilikuwa nimekiacha nyuma. Kijiji changu? Hisia hizi zilinifanya nirudi nyuma. Lakini wakati wote moyo uliniambia kuwa lazima kulikuwa na mtu karibu nami (uk.100).

Tunabainishiwa kuwa dhamiri ya mtu haisababishwi na fikra zake, bali moyo wake. Anapoelezea kuhusu mabadiliko ya siasa na uchumi, hususani wakati wa ujio wa Usoshalisti, anatueleza kuwa “watu wakawa na moyo wa kujitolea na kushirikiana (uk. 79).” Tumeshabainisha kuwa fikra zao hujengwa moyoni, hawazungumzii nafasi ya ubongo katika kufikiri. Haya tunaelezwa na mwandishi, kupitia mhusika Mimi. Anasema:

Hivyo ndivyo tulivyoendelea kuishi na Mzee. Yalikuwa maisha ya kuambizana ukweli, kukaripiana wakati mwingine, kuchekeana na kujadiliana yaliyokuwa mioyoni mwetu (uk.111).

Mbali na nukuu hii kutumulikia kuhusu nafasi ya moyo katika kuibua fikra, pia inatuyakinishia umadhubuti wa msingi wa Nadharia ya Epistemolojia inayosisitiza kuwa maarifa hupatikana kutokana na kujua na tajiriba. Tajiriba ni uzoefu; uzoefu hupatikana kwa mtu kufanya au kukabiliana na jambo kwa muda mrefu. Msomaji anapoendelea kusoma kitushi hiki cha Mimi kukutana na Mzee, inamfunukia kuwa uhusiano wao ulikuwa unaimarika kadri walivyoendelea kuishi. Ilimchukua Mimi muda mrefu tangu hali ya kusitasita iliyomtokea siku ya mwanzo alipokuwa anakikaribia kibanda cha Mzee hadi kufikia hatua ya ‘kuchekeana’ naye. Kuchekeana huko ni ithibati ya kuzoeana, kuelewana, na kuendana katika malengo. Lengo kubwa la Mimi lilikuwa kujifunza kuhusu kweli za maisha.

Mwandishi anaendelea kutujuza nafasi ya moyo katika kujenga haiba ya mtu. Kwa kutumia kinywa cha Mzee, tunaambiwa:

Na bado anavumisha jina lake kama mwanasayansi na mvumbuzi mkubwa atakayeokoa ulimwengu huu na taifa zima la binadamu. Mdomo wake hautulii mara hili mara lile. Ningemfunza adabu! Ila uzuri wake mmoja – bado anao moyo wa huruma, kama wewe hapa (uk.109).

Maelezo haya yanaonesha namna moyo unavyojibainisha kama kitambulishi cha utu wa mtu. Ni muhimu tuweke bayana hapa kuwa moyo kama kibainishi cha mtu ni dhana ya kisaikolojia. Hii ni kwa kuwa haionekani, bali kinachoonekana ni matokeo yake. Matokeo hayo ni tabia inayojibainisha kwa kuwa na moyo mwema au mbaya.

Tunapochunguza fikra za mwandishi kuhusu moyo na dhima zake, tutabaini kuwa mambo haya mawili, kwa pamoja, yametumika kumgawanya mtu katika mitazamo miwili, yaani, “mtu-kweli” na “si-mtu.” Mwandishi ameonesha tabia kama matokeo ya moyo wa mtu. Anatufundisha tuwe na tabia ya kufikiri kwa njia ya kuutafakari ulimwengu ili kuupata ukweli kuhusu maisha. Tunaelezwa kuwa kuutafiti ulimwengu kwa njia ya tafakuri siyo jambo la siku moja. Ni safari ndefu inayohitaji tabia ya ushujaa na ujasiri wa hali ya juu. Hii ni kwa kuwa safari hiyo ina vikwazo vingi.

Mwongozo wa mtunzi kuhusu tabia inayombainisha Mbantuu kama mtu-kweli umefungwa kwenye motifu ya safari. Anatueleza kuwa “moyo wa ujasiri, moyo wa udadisi na utundu ulinisukuma mbele. Nilitaka kujua kilichokuwa nyuma ya miba

hiyo!” (uk.11). Hapa, Mimi anayakinisha fikra za Nadharia ya Epistemolojia kuwa vyanzo vya kujua hutofautiana. Maarifa kuhusu maisha yanapatikana katika vyanzo mbalimbali. Mwandishi anatuonesha kuwa Mimi anayasaka kutoka kwenye ‘miba’. Kulingana na utafiti wetu, ‘miba’ ni jazanda ya matatizo, mazingira au vikwazo mbalimbali ambavyo mwanadamu anavipitia maishani.

Mimi, ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya ya *Mzingile*, anaendelea kutuongoza katika harakati za kuutafuta ukweli kuhusu maisha. Tunaoneshwa kuwa anafanya hivyo kwa ujasiri, udadisi na utundu. Mambo haya matatu ambayo yanaongozwa na moyo ni zana za kuwezesha kufikiri. Kwayo, Mimi anaweza kuvuka vikwazo kadhaa bila ya kukata tamaa ya kuhakikisha ukweli unapatikana. Tunaoneshwa kuwa dhima hizo tatu zinabebwa na moyo wake. Kupitia dhima hizo, Mimi anaonekana mtu-kweli toka mwanzo hadi mwisho wa hadithi hii. Anaendelea kusema:

Juu ya kilele hiki niliweza sasa kuona kitu kama nyumba... Nyumba hii ilikuwa imejengwa juu ya mwamba mmoja mkubwa. Mwamba huu ulikuwa juu ya mawe mengine makubwa. Ilikuwa vigumu kuufikia... Nilipumzika kwa muda wa siku mbili. Nilifikiria namna ya kuifikia nyumba hiyo ambayo haikuonesha kuwa na dirisha... Moyoni nilikuwa nikijiuliza, “Aliyeyenga alifikaje (uk.17)?”

Maelezo haya yanathibitisha kuwa tabia za ujasiri, udadisi na utundu ndizo zinazoweza kumfanya mtu asikate tamaa. Tabia hizo, kwa mujibu wa data hii, zinachagizwa na moyo.

Katika mwendelezo wa kuonesha jinsi moyo unavyoleta ujasiri na uthubutu, Mzee anamwambia Mimi aliyejusurishwa na moyo wake hadi kufanikiwa kumfikia yeye (Mzee) kuwa “watu kwa muda wa karne nyingi, wamesita kuingia humu (ndani ya nyumba yangu) kwa nguvu, nguvu zao wenyewe (uk. 20) (msisitizo kwenye mabano ni wetu).” Kwa ujasiri, udadisi na utundu unaosababishwa na moyo, tunaelezwa kuwa tusiogope kufa. Tujitoe kwa manufaa ya jamii yetu. Hii ni kwa sababu “ujasiri wa mja hukamilishwa na kifo (uk. 24).”

Katika riwaya nyingine, *Dunia Uwanja wa Fujo* (Kezilahabi, 2007), mwandishi anaendelea kutuonesha kuwa moyo ndio utunzao fikra na kuzalisha tafakuri tofauti kuhusu ulimwengu. Mwandishi anasema “Mungere alimwomba Leonila na Aurelia walale naye nyumba moja... Mungere alianza kuwaambia yaliyokuwa moyoni mwake (uk. 6).” Anayosema Mungere yanatoka moyoni na siyo akilini mwake. Kisayansi, ubongo ndio huzalisha fikra na kutunza kumbukumbu; hata hivyo, kwa Wabantu hiyo ni kazi ya moyo. Nkulu-N’Sengha (2005) anaonesha namna Wabantu wanavyoutazama ulimwengu wao wanapouzungumzia moyo. Anasema:

*In most Bantu languages, the word heart also stands for thought” and “a muntu wa mucima muyampe” is not only a person with a good heart in the sense of being kind, compassionate, and generous but also a person of good thought (uk. 42).*

Katika lugha nyingi za Kibantu, neno moyo pia huwakilisha fikra na “a muntu wa mucima muyampe” (tungo ya Kiluba inayomaanisha mtu mwenye moyo mzuri) siyo tu ni mtu mwenye moyo mzuri kwa maana ya kuwa mwema, mkarimu, na mwenye huruma, bali pia mtu mwenye mawazo mazuri (ikiwamo busara au hekima) (tafsiri yetu, ufafanuzi wa kwenye mabano ni wetu pia).

Hii ni ithibati nyingine muhimu kuhusu namna moyo ambao ni kibainishi cha mtu unavyofungamanishwa na dhana hizo za kiepistemolojia.

Kezilahabi anazidi kusisitiza kuhusu nafasi ya moyo kama mhimili wa epistemolojia ya Wabantu kuhusu ontolojia yao kwa kutueleza kuwa “Leonila alimtaazama dada yake usoni akionesha alama za kutafuta msaada, hakufahamu hata namna ya kuanza hadithi ambayo alikuwa amekwishaikariri moyoni” (uk. 6). Hadithi haikukaririwa ubongoni, akilini, wala kichwani kama ambavyo wengi tungetegemea aandike, bali imekaririwa moyoni.

Zaidi, tunaoneshwa nafasi ya moyo katika uga wa epistemolojia na ontolojia wakati Tumaini akiwa katika lindi la mawazo kuhusu ulimwengu wake. Kalamu ya Kezilahabi inatueleza:

Akiwa njiani kurudi nyumbani, Tumaini alisikia sauti kama ya ndege akiimba kwa huzuni: “Tumaini usidhani kwamba umefanya jambo zuri. Huyu mzee amekwisha kuwa kama mtoto mdogo. Wewe umemchezea kama picha. Tumaini, hii ndiyo heshima yako kwa watu kama hawa! Tumaini huna huruma; utakuja kuwa kama yeye siku moja!” Hiyo haikuwa sauti ya ndege. Sauti ya moyo wake ndiyo iliyokuwa ikimsumbua (uk. 19).

Anachokifanya Tumaini hapa na kuwasilishwa na mwandishi ndicho wafanyacho Wabantu wawapo kwenye tafakuri nzito kuhusu maisha yao. Katika hali hiyo, husemwa kuwa Wabantu ‘huzungumza’ na mioyo yao. Katika nukuu hii, mwandishi anatumia kinywa cha Tumaini kuwakumbusha Wabantu kuhusu hatua za kuliendea duara la kiontolojia. Pia, kuna onyo la kiontolojia na ukumbusho kwa watu kama Tumaini kuhusu kutafakari athari za matendo wayatendayo wakiwa katika rika la ujana. Kidole cha ole kilichomo katika nukuu hii kinaoneshwa kwa ‘Tumaini’ mwingine yeyote



aliyepo katika jamii ambaye anawafanyia matendo mabaya wazee kuwa, ‘...kuwa na huruma, siku moja utakuja kuwa kama yeye (mzee)’.

Kitushi cha Tumaini na nafasi ya moyo wake katika kutafakari maisha kinaendelea kwa hadhira ya riwaya hii kuelezwa: “Tumaini alikuwa amekusudia kumchukua Anastasia bila idhini ya wazazi wake—sawa na kuiba—alisema moyoni” (uk. 46). Kilichomo moyoni hujulikana na mwenye moyo, lakini matokeo ya moyo huo huwa dhahiri. Wabantu hutumia hicho kinachodhihirishwa kumweka mtu katika kundi la mtu-kweli au si-mtu. Tunaelezwa dhamiri ya Tumaini ilikuwa moyoni mwake, ndiyo maana, “bila kufahamu hila aliyokuwa nayo Tumaini moyoni mwake, Mulele na Bukehele walijiandaa kwa harusi... (uk. 47). Tunachoaridhiwa hapa kupitia hila za Tumaini ni kwamba, hakuwa mtu mwema (si-mtu).

Ontolojia ya mtu mwenye moyo wa hila huwaje? Kezilahabi anajibu swali hili kwa kutuaridhia yaliyokuwa yanadhihirishwa na moyo wa Tumaini. Anaeleza kuwa, toka wakati wa ujana wake amekuwa akidhihirisha hila hiyo ya kukosa wema, kuwa na ujeuri, dharau na majivuno. Katika riwaya hii ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, tunaoneshwa kuwa Tumaini alipenda sana mambo ya ngono. Katika ukurasa wa 8, tunaoneshwa kuwa alipenda kusoma kitabu cha mapenzi kilichoitwa *Sex and You*. Nadharia alizopata kitabuni humo ‘zinazaa matunda’ kwa kusababisha mimba kwa Leonila, mmoja wa mabinti aliozini nao. Mzazi wa binti, Mungere, alipoamua kumfuata Tumaini nyumbani kwake ili kuzungumzia suala la mimba ya Leonila, tunafunguliwa zaidi kuhusu tabia ya Tumaini (ambayo ni matokeo ya mifanyiko ya moyoni kwake). Tunaelezwa:

Tumaini alipomwona Mungere, alifahamu mara moja jambo lililomleta. Alitaka kumtukana, lakini Mungere aliingia ndani ya nyumba kwa upole vile kwamba Tumaini alipofunua mdomo, maneno yalimkwama kooni (uk. 8).

Pamoja na kuwa katika tukio hili Tumaini alisita kumtukana Mungere, hatimaye aliweza kulifanya jambo hilo alipokuwa anaonywa na walimu wake shuleni walipomuadhibu. Aliwatukana, “Washenzi ninyi! Baba hajapata kunipiga! Mna haki gani ninyi ya kunipiga (uk. 10).” Vilevile, tunaelezwa kuwa “Kijiji hakikufahamu kwamba mawazo ya Tumaini yalikuwa ni upinde kwa utamaduni wao na upanga kwa wajukuu wao (uk. 16).” Huyu ndiye Tumaini mwenye moyo wenye hila. Tabia yake inaoneshwa wazi ikikiuka mila na desturi za jamii yake. Hapa, tunaingizwa na mwandishi katika mjadala wa maadili. Ni muhimu tusesitize hapa kuwa jambo lolote linaloashiria kukiuka mila na desturi huwa linafikiriwa katika misingi ya kiontolojia. Kutokiuka mila na desturi kuna maana ya kuimarisha kani-uhai na kuwa sehemu imara ya duara la maisha; kinyume chake ni kuwaudhi wahenga.

Kwa jumla, Tumaini alikuwa si-mtu katika kipindi fulani cha maisha yake. Mwandishi anatuonesha kuwa tabia ya binadamu si jambo aushi. Mwendelezo wa masimulizi ya matukio ya riwaya hii ya *Dunia Uwanja wa Fujo* unatubainishia kuwa, baadaye Tumaini alibadilika. Hatimaye, akawa mtu-kweli.

#### 4. Hitimisho

Mjadala kuhusu nafasi ya moyo katika epistemolojia ya Wabantu kuhusu ontolojia yao umethibitisha kuwa moyo ni miongoni mwa vibainishi vya mtu kwa mujibu wa maarifa ya Wabantu. Aidha, mjadala umeonesha kwamba licha ya kuwa moyo ni kibainishi cha mtu kiontolojia, pia ni kielelezo cha kiepistemolojia, ambapo kazi yake kubwa ni kumwongoza mtu kufanya tafakuri kuhusu ulimwengu wake. Hii ina maana kwamba Wabantu wanaamini kwamba fikra hujengwa moyoni na siyo akilini. Hatimaye, makala hii imethibitisha kwamba moyo alionao mtu ndio ubebao tabia yake kwa jumla; na kuwa kipimo kinachowawezesha Wabantu wamweke kwenye mizani inayowaweka katika makundi makubwa mawili, yaani, ‘watu-kweli’ na ‘si-watu.’ Hii ina maana kwamba matendo na haiba ya mtu huongozwa na moyo wake. Kwa hiyo, kupitia utendaji unaosababishwa na moyo, mtu huweza kuiimarisha au kuidhoofisha kani-uhai. Kwa mtazamo huu, moyo nao huonekana hufikiriwa kiontolojia na Wabantu.

#### Marejeleo

- Adeofe, L. (2004). Personal identity in African metaphysics. In L.M. Brown (Ed.), *African philosophy: New and traditional perspectives*, pp. 69-83. Oxford: Oxford University Press.
- Anthony, K. (2009). *Descartes: A study of his philosophy*. South Bend, IN: St. Augustine’s Press.
- Appiah, K.A. (1992). *In my father’s house: Africa in the philosophy of culture*. Oxford: Oxford University Press.
- Ayers, M. (1991). *Locke: Epistemology and ontology*. London: Routledge.
- Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika riwaya za Shaaban Robert*. Dar es Salaam: TUKI.
- Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika muktadha wa epistemolojia ya Kibantu*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (haijachapishwa). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.

- Cottingham, J. (2010). Between two worlds: A reading of Descartes's *Meditations*, by John Carriero. *Mind*, 119(475): 786–789. <https://doi.org/10.1093/mind/fzq046>
- Cottingham, J. (2017). *Translation of Descartes' meditations on first philosophy*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Duwe, M. (2022). *Uchimuzi wa eskatolojia ya Waafrika katika fasihi simulizi: Mifano kutoka katika mbolezi za jamii ya Wangoni*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (hajachapishwa). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Gbadegesin, S. (1984). Destiny, personality and the ultimate reality of human existence: A Yoruba perspective. *Ultimate Reality and Meanings*, 7(3):173-188. <https://doi.org/10.3138/uram.7.3.173>
- Gbadegesin, S. (1991). *African philosophy: Traditional Yoruba philosophy and contemporary African realities*. New York: Peter Lang.
- Griswold, C.L. (2001). *Platonic writings/Platonic readings*. London: Penn State Press.
- Gyekye, K. (1995). *An essay on African philosophical thought: The Akan conceptual scheme*. Philadelphia, PA: Temple University Press.
- Hallen, B., & Sodipo, J.O. (1997). *Knowledge, belief and witchcraft: Analytic experiments in African Philosophy*. Palo Alto, CA: Stanford University Press.
- Kagame, A. (1989). The problem of 'man' in Bantu philosophy. *Journal of African Religion and Philosophy*, 1(1): 35-40.
- Kaphagawani, D. (2004). African conceptions of a person: A critical survey", In K. Wiredu, (Ed.), *Companion to African Philosophy*, pp. 332-334. Malden, MA: Blackwell Publishing.
- Kaphagawani, D., & Malherbe, J.G. (2003). African epistemology. In P. H. Coetzee & A.P.1. Roux (Eds.), *The African philosophy reader*, pp. 205-16. London: Routledge.
- Kasprisin, L. (1987). Literature as a way of knowing: An epistemological justification for literary studies. *Journal of Aesthetic Education*, 21(3):17-27. <https://doi.org/10.2307/3332867>
- Kezilahabi, E. (2007). *Dunia uwanja wa fujo*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.
- Kezilahabi, E. (2008). *Kichwamaji*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers,.
- Kezilahabi, E. (2011). *Mzingile*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.
- Kezilahabi, E. (2011). *Nagona*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

- Khamis, T. Y. (2022). *Mdhihiriko wa ontolojia ya Wazanzibari katika riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka riwaya teule za Muhammed Said Abdulla*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (haijachapishwa). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mbatiah, A.M. (1998). Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: Nagona na Mzingile. *Mulika* 24: 1-12. TUKI, Dar es Salaam.
- Mbiti, J.S. (1995). *African religion and philosophy*. London: Heinemann.
- Mihanjo, A. (2004). *Falsafa ya usanifu wa hoja kutoka Wayunani hadi Watanzania (Waafrika)*. Morogoro: Salvatorianum.
- Mtega, W.S. (2023). *Uchimuzi wa kosmolojia katika tambiko: Uchunguzi katika ushairi wa matambiko ya Wapangwa*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Newman, L. (2023). Descartes' epistemology. In E.N. Zalta, & U. Nodelman (Eds.), *The Stanford encyclopedia of philosophy* (Winter 2023 edition), <https://plato.stanford.edu/archives/win2023/entries/descartes-epistemology>
- Nkulu-N'Sengha, M. (2005). African epistemology. In M. Asante, & A. Mazama (Eds.), *Encyclopedia of Black studies*, pp. 39-44. Thousand Oaks, CA: SAGE Publications.
- Onyeowuenyi, I. (1995). "Is there an African philosophy?," In A.G. Mosley (Ed.), *African philosophy: Selected readings*. New Jersey: Prentice-Hall.
- Ponera, A.S. & Mkomwa, S. (2019). Utanzuaji wa Vibandiko kama Mkakati wa Kuzielewa Riwaya za Kifalsafa: Mfano wa Riwaya ya Nagona. Katika A.S. Ponera na Z.A.Badru (Wah.), *Koja la taaluma za insia: Kwa heshima ya Profesa Joshua S. Madumulla* (459-480). Dar es Salaam: Karljamer Publishers.
- Stumpf, S.E. & Abel, D.C. (2002). *Elements of philosophy: An introduction*. New York: McGraw Hill.
- Tempels, P. (1959). *Bantu philosophy*. Paris: Presence Africaine.
- Wiredu, K. (1980). *Philosophy and an African culture*. Cambridge: Cambridge University Press.

---

## ABOUT THE AUTHORS

### **Athumani Ponera**

Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

**Email:** athuman.ponera@udom.ac.tz

---

Dr. Athumani S. Ponera is a Senior Lecturer of Swahili Studies. He is working with the Department of Kiswahili of the University of Dodoma, Tanzania. His academic interests are in the following areas: prose works, comparative literature, folk studies, and qualitative research.

### **Issaya Lupogo**

Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania

**Email:** islupogo@mzumbe.ac.tz

---

Dr. Issaya Lupogo holds a PhD in Kiswahili, a Master of Arts in Linguistics (English), and a Bachelor of Arts in Education (Kiswahili and English). All degrees were attained at the University of Dar es Salaam, Tanzania. Currently, he is a lecturer in the Department of Languages and Communication Studies at Mzumbe University, Tanzania, where he coordinates Kiswahili and English courses in linguistics. He is also a consultant in translation, language editing, qualitative research, and teaching methodologies.

---